**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS MIPANGO NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**24 APRILI, 2025**

# YALIYOMO

**SEHEMU YA KWANZA** ... 1
**1.0 UTANGULIZI** ... 1
1.1. Maelezo ya Awali ... 1
1.2. Msingi wa Uchambuzi ... 2
1.3. Mawanda ya Uchambuzi ... 3
SEHEMU YA PILI ... 4
2.0 **MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHIMINI** ... 4
2.1 Ufafanuzi wa Jumla ... 4
2.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli ... 4
2.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Bajeti ... 6
2.3.1 Fungu Na. 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina ... 6
2.3.2 Fungu Na. 11- Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji ... 7
2.3.3 Fungu Na. 66 – Tume ya Mipango ... 8
2.4 Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Ofisi ya Rais, ... 10
2.5 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ... 11
2.6 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ... 13
**SEHEMU YA TATU** ... 14
**3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** ... 14
3.1 Maduhuli ... 14
3.2 Matumizi ya Kawaida ... 15
3.3 Miradi ya Maendeleo ... 16
**SEHEMU YA NNE** ... 19
**4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI** ... 19
4.1 Maoni ya Jumla ... 19
4.2 Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina ... 19
4.3 Fungu 011 - Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ... 20
4.4 Ushauri Mahususi Fungu kwa Fungu ... 20
4.4.1 Fungu 66 – Tume ya Mipango ... 20
4.4.3 FUNGU NA 011-Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji ... 22
**5.0 HITIMISHO** ... 23

# ORODHA YA MAJEDWALI

**JEDWALI NA. 1:** Makusanyo ya Maduhuli 2024/2025............................................ 5

**JEDWALI NA. 2:** Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2024/2025 ................. 9

**JEDWALI NA. 3:** Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2024/2025 ................ 10

**JEDWALI NA. 4:** Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha 2024/2025 .......... 11

**JEDWALI NA. 5:** Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026............................................. 14

**JEDWALI NA. 6:** Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2025/2026 ............... 15

**JEDWALI NA. 7:** Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2025/2026 ................ 17

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

---

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1. Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kukidhi masharti yaliyokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;
b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;
c) Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;
d) Sehemu ya Nne inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na
e) Sehemu ya tano ni Hitimisho.

### 1.2. Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Uratibu ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kifungu cha 6(2)(b) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na

Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

### 1.3. Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu matatu (3) ambayo ni: -

a) **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina;

b) **Fungu 11** - Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji; na

c) **Fungu 66** – Tume ya Mipango

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHIMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu matano yaliyochambuliwa kama ifuatavyo; -

(a) Makusanyo ya maduhuli;
(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya kawaida na Bajeti ya Maendeleo;
(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji;
(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na
(e) Ulinganisho wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

### 2.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2024/25, ilikadiria kukusanya mapato yasiyo ya kodi kiasi

cha **Shilingi 1,113,949,673,000.00** kupitia Fungu Na. 07 Ofisi ya Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kuwa Ofisi hii kupitia Fungu Na. 07 hadi kufikia mwezi Februari, 2025 Ofisi imekusanya kiasi cha **Shilingi 562,585,408,207.53** sawa na **asilimia 51** ya lengo la mwaka.

**Mheshimiwa Spika** Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa kuweza kuongeza Ukusanyaji wa Mapato ukilinganisha na mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo hadi kufikia Februari 2024 Wizara ilikusanya Maduhuli kwa **asilimia 37** ya makadirio.

Aidha, mchanganuo wa maduhuli kwa Fungu Na. 07 unaoneshwa katika **Jedwali Na. 1.**

**JEDWALI NA. 1: Makusanyo ya Maduhuli 2024/2025**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | MAKUSANYO YA MADUHULI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|
| **Fungu 07** – Ofisi ya Msajili Wa Hazina | 1,113,949,673,000 | 562,585,408,207.53 | **51** |
| **JUMLA KUU** | 1,113,949,673,000 | 562,585,408,207.53 | **51** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba bado ukusanyaji wa maduhuli unaendelea na hadi itakapofika robo tatu na nne ya mwaka huu wa fedha unaoisha Wizara kupitia Msajili wa Hazina watakuwa wameweza kufikisha lengo kwakuwa gawio na michango kutoka kwenye mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa ambao kwa utaratibu uliopo gawio hutolewa kipindi hiko kwa kila mwaka**.**

**Mheshimiwa Spika**, Aidha Kamati ilielezwa kwamba Sehemu kubwa ya Ukusanyaji wa Maduhuli hadi kufikia Februari, 2025 unatokana na Kodi za Upangishaji, Michango ya asilimia 15 ya Mapato Ghafi, Gawio, Marejesho ya TTMS, Rejesho la Riba na Mikopo, Ziada na Malipo mengineyo na Ukusanyaji wa Madeni ya EX-NBC na Ubinafsishaji.

### 2.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Bajeti

#### 2.3.1 Fungu Na. 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa Fedha 2024/25, Ofisi ya Msajili wa Hazina iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 167,895,468,325.00** baada ya uhamisho wa **Shilingi 115,513,345,325.00** ambayo ilitoka Wizara ya fedha ambayo iliwasilishwa Mamlaka ya Ngorongoro kwa ajili ya kutekeleza zoezi la uhamisho wa wananchi kutoka Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro.

**Mheshimiwa Spika** kati ya fedha hizo zilizoidhinishwa, **Shilingi 7,305,056,000** zilitengwa kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi**

**159,300,754,325** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 1,289,658,000.00** kwa ajili ya Fedha za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 132,106,065,459.31** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida sawa na **asilimia 83** ya bajeti iliyoidhinishwa, ambapo kati ya fedha hizo **Sh. 4,069,756,537.04** ni kwa ajili ya Mishara **na Sh. 128,036,308,922.27** ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo ambapo kati ya fedha hizo za matumizi Mengineyo **Sh. 117,702,209,549.57** ni kwa ajili ya matumizi maalum na **Sh. 10,334,099,372.70** ni kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi. Aidha **Sh. 970,188,000.00** sawa na **asilimia 75** zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

### 2.3.2 **Fungu Na. 11- Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 30,216,547,238.00**, kati ya fedha hizo **Sh. 18,632,828,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 6,774,092,000.00** ni Mishahara (PE) na **Sh. 11,858,736,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 11,583,719,238.00** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 15,290,692,815.34** sawa na asilimia **51** ambapo **sh. 11,804,354,730.34** sawa na **asilimia 63.3** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 4,436,098,062.00**

ni kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh.7,36,256,668.34** ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo(OC), na **Sh. 3,486,338,085.00** sawa na **asilimia 30** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

### 2.3.3 Fungu Na. 66 – Tume ya Mipango

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 46,221,630,000.00**, kati ya fedha hizo **Sh. 37,806,250,000.00,** sawa na **asilimia 82** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 3,806,250,000.00** ni Mishahara (PE) na **Sh. 34,000,000,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 8,415,380,000.00** sawa na **asilimia 18.2** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 23,100,442,792.08** sawa na asilimia **50** kati ya fedha hizo **sh. 22,384,992,792.08** sawa na **asiliimia 48.4** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida ambapo kati ya fedha hizo **Sh. 1,962,782,480.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh.20,422,210,312.08** ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo(OC), na **Sh. 715,450,000.00** sawa na **asilimia 8.5** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba Upatikanaji wa Fedha kwa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa Fedha 2024/25 ni wa kuridhisha ukilinganisha na mwaka wa fedha 2023/24 ambapo

hadi kufikia februari 2024 hakuna Fungu ambalo liliweza kupata fedha kwa Uwiano wa Asilimia 66.6

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kupeleka fedha kwa wakati kwenye Wizara hii muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu la Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kuwa inatekeleza majukumu yaliyowekwa kisheria kikamilifu ili kuhakikisha kwamba Taifa letu linakuwa na vyanzo imara vya mapato ambavyo vitatuondosha na kuwa tegemezi kwa fedha nje.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha hizo kwa Mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2** na **Jedwali Na. 3**.

**JEDWALI NA. 2: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2024/2025**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | 159,300,754,325 | 132,106,065,459.31 | 84 |
| **Fungu 11** – Ofisi ya Rais,Mipango na Uwekezaji | **18,632,828,000.00** | **11,804,354,730.34** | 63.5 |
| **Fungu 66** – Tume ya Mipango | **37,806,250,000.00** | **22,384,992,792.08** | 59.21 |
| **JUMLA KUU** | **181,714,207,325** | **166,295,412,981.73** | **91.5** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**JEDWALI NA. 3: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2024/2025**

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | **1,289,658,000.00** | **970,188,000.00** | 75 |
| **Fungu 11**– Ofisi Rais Mipango na Uwekezaji | **11,583,719,238.00** | **3,486,338,085.00** | 48.58 |
| **Fungu 66** – Tume Mipango | **8,415,380,000.00** | **715,450,000.00** | 8.5 |
| **JUMLA KUU** | **21,288,757,238.00** | **5,171,976,085.00** | **24** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ni wa kuridhisha, isipokuwa katika miradi ifuatayo;

a) **Fungu Na. 66 – Tume ya Mipango**

**Mradi Na. 2229: Enhancement of Institutional Capacity and Research** ambao ulitengewa **Sh. 8,000,000,000.00,** ambapo hadi Kufikia Februari 2025 Miradi huu ulipokea Jumla ya **Sh. 300,070,000.00** sawa na **asilimia 3.75** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

## 2.4 Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Ofisi ya Rais,

**Mheshimiwa Spika**, bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taasisi zilizopo chini ya Ofisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa Matumizi unaoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyoombewa fedha kwa mwaka wa Fedha 2024/25

## 2.5 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara na taasisi zilizo chini ya ofisi hii ziliidhinishiwa jumla ya **Sh 21,288,757,238.00**kwa Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika **Jedwali Na. 4**

**JEDWALI NA. 4: Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha 2024/2025**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 |
|---|---|---|
| **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | **NA. 6251** Programu ya maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma | 1,289,658,000.00 |
| **Fungu 11** – Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji | **NA. 4429** Institutional Support<br>**NA 4933** Export Processing Zone Development<br>**NA 4920** Tanzania Mini Tiger Plan 2020<br>**NA. 4901** Implementation of BEST Programme | 1,896,549,000.00<br>5,410,226,000.00<br>1,314,506,000.00<br>3,406,726,000.00 |
| **Fungu 66** – Tume ya Mipango | **NA. 2229** Enhancement of Institutional Capacity and Research<br>**NA. 2229** Enhancement of Institutional Capacity and Research | 8,000,000,000<br>415,380,000 |
| **JUMLA KUU** | | **21,288,757,238.00** |

***Chanzo****: Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji   na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika** Kamati ilitembelea mradi mmoja kati ya Miradi saba (7) inayotekelezwa na Ofisi hii kwa kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 na kuchambua utekelezaji wa mradi huo kama ifuatavyo:-

**Mradi Na. 4933:** Ujenzi wa Ofisi ya Kanda maalumu ya Kiuchumi ya Benjamini Mkapa-Benjamin Mkapa Special Economic Zone, Dar Es salaam.

**Mheshimiwa Spika** Mradi huu unahusu ujenzi wa Uzio ambao unatenganisha eneo la viwanda na eneo la kupooza umeme na ukarabati wa mifereji ya maji ya Mvua katika ukanda Maalumu wa Kiuchumi wa **Benjamin William Mkapa (BWM Special Economic Zone).**

**Mheshimiwa Spika** Mradi huu ulipokea pesa kiasi cha **Shilingi 149,900,530** mnamo mwezi **Disemba 2023** na ulianza kutekelezwa kuanzia **19 Februari 2024** na ulikamilika **Agosti 2024** na kukabidhwa kwa Serikali tarehe **20 Novemba 2024**.Aidha Kamati ilielezwa kwamba mradi huu ulitekelzwa kwa kutumia utaratibu wa **FORCE ACCOUNT.**

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile Kamatii ilitembelea baadhi ya wawekezaji ambao wanasimamiwa na Mamlaka ya Uwekezaji wa Maeneo Maalumu ya Kiuchumi waliopo katika eno hilo la **Benjamin Mkapa Special Ecomnomic zone** ambao walionesha

kufurahishwa na usimamizi wa Wizara kwao kama wawekezaji. Aidha walikua na maombi kwa Serikali kushirikiana na Taasisi za kifedha kuwa na dirisha la kutoa mikopo kwa wamiliki wa viwanda ya kuongeza thamani ya bidhaa zao ilikuweza kushindana na bei ya soko la dunia.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha Kamati inampongeza **Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan** kwa namna ambavyo anaendelea kufungua milango kwa wawekezaji nchini na kutafuta fursa kwa wawekezaji wazawa, hali hii inadhihirisha namna ambavyo Serikali ya awamu ya Sita imedhamiria kukuza Sekta ya uwekezaji nchini.

## 2.6 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 3.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Sh. 1,566,260,545,635.00** ikilinganishwa na **Sh. 1,168,543,413,000.00** katika Mwaka wa Fedha **2024/2025** kama ambavyo imeainishwa katika **Jedwali Na. 5**. Hii ni na sawa na ongezeko la **asilimia 25.4** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha unaoisha.

**JEDWALI NA. 5: Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 |
|---|---|---|
| **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | 1,168,543,413,000.00 | **1,566,260,545,635.0** |
| **JUMLA KUU** | **1,168,543,413,000.00** | **1,566,260,545,635.00** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba ongezeko hilo la makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha **2024/2025** litatokana na uimarishaji wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ya Msajili wa Hazina ambayo itaongeza usahihi wa takwimu za upatikanaji wa mapato na mashirika ambayo serikali ina hisa au kutegemea kupata gawio na

kurahisisha utoaji taarifa na ufatiliaji wa mapato na matumizi ya Mashirika.

## 3.2 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 122,122,585,000**Ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 22,525,101,000**ni mishahara, na **Sh. 99,597,584,000**ni matumizi mengineyo, kama ambavyo imechanganuliwa katika **Jedwali Na. 6**

**JEDWALI NA. 6: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2025/2026**

| FUNGU | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA |
|---|---|---|---|
| **Fungu 07** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | 8,662,948,000.00 | 51,922,183,000.00 | 60,585,131,000.00 |
| **Fungu 11**– Ofisi Rais Mipango na Uwekezaji | 8,716,784,000.00 | 13,675,401,000.00 | 22,392,185,000.00 |
| **Fungu 66** – Tume ya Mipango | 5,145,369,000.00 | 34,000,000,000.00 | 39,145,369,000.00 |
| **JUMLA KUU** | **22,525,101,000** | **99,597,584,000** | **122,122,585,000** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepungua kwa kiasi cha **Sh. 59,591,622,325** sawa na **asilimia 33** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi

ya kawaida ndani ya ukomo bajeti ilikuwa **Sh. 181,714,207,325 ikiwa na baada ya ongezeko la kiasi** cha Shilingi **115,513,345,325.00** ambayo ilitoka Wizara ya fedha na iliwasilishwa kwa Mamlaka ya Ngorongoro kwa jili ya kutekeleza zoezi la uhamisho wa wananchi kutoka Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria.

### 3.3 Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 26,507,276,000.00** kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 14,553,437,000.00** ni fedha za ndani, na **Sh. 11,953,839,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **Sh. 5,218,518,762.00** sawa na **asilimia 19.6** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha, sababu ya kuongezeka kwa bajeti kumechangiwa na mpango wa

Serikali kuhakikisha kwamba kuna maendeleo endelevu kwa watanzania wote kwa kuhimiza mipango madhubuti na Uwekezaji nchini. Kama ambavyo imechanganuliwa katika **Jedwali Na. 7.**

**JEDWALI NA. 7: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2025/2026**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | |
|---|---|---|---|
| | | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 07** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | **NA. 6251** Programu ya maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma | 370,691,000 | 1,300,000,000 |
| **Fungu 11**– Ofisi ya Rais,Mipango na Uwekezaji | **NA 4901** Implementation of BEST Programme | | 5,372,130,823 |
| | **NA. 4904** Financial Access for sustainable and Transformationa;(FAST) Growth Project | | 2,420,431,177 |
| | **NA 4920** Tanzania Mini Tiger Plan 2020 | 2,747,906,800 | |
| | **NA 4933** Export Processing Zone Development | 788,703,600 | |
| | **NA.**6251 Public Finance Management Reform Programme (PERMP) | | 1,062,102,000 |
| | **NA.**6260 Institutional Support | 6,582,881,000 | |
| **Fungu 66** – Tume ya Mipango | **NA. 2229** Enhancement of Institutional Capacity and Research | 7,566,093,328 | 0 |
| | **NA 6251** PFMRP VI | 433,906,672 | 779,074,600 |
| | **NA 6526** National Population Project | | 582,202,400 |

| | | |
|---|---|---|
| **Jumla Ndogo** | **14,553,437,000** | **11,953,839,00** |
| **JUMLA KUU** | **26,507,276,000.00** | |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza Miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani, Aidha Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kupitia Wizara hii kuhakikisha kwamba Fedha zote zinazotengwa kwa ajili ya Utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinapatikana kwa wakati, zinatekeleza miradi iliyopangwa kutekelezwa ili kuweza kuleta tija na ustawi wa wananchi kwa ujumla.

**SEHEMU YA NNE**

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa ofisi kujiwekekea malengo ya ukusanyaji maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji, na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

### 4.2 Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina

(i) Kukokuwa na Uwekezaji wa kimkakati katika masoko ya Hisa na Taasisi Binafsi zenye tija na manufaa kwa Taifa, Serikali itakosa gawio ambalo linaweza kutumika kwa maendeleo ya Nchi;

(ii) Mali zilizorejeshwa serikalini zisipofanyiwa tathimini zinasabishia Serikali upotevu wa fedha kwa kushindwa kujua thamani halisi ya mali hizo;

(iii) Ofisi ya Msajili wa Hazina kutokuwa na usimamizi Madhubuti wa mashirika ya Umma kunachangia kukosekana kwa gawio kwa serikali na kupunguza mapato ambayo yangeingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

(iv) Kutokuwepo kwa makadirio ya makusanyo ya maduhuli yanayoakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya

vyanzo vyake hupelekea kuonekana kuwa hakuna tathmini ya kutosha juu ya vyanzo hivyo vya ukusanyaji wa maduhuli; na

(v) Madeni yanayotokana na ubinafsishaji wa mali za Serikali ili kuboresha na kuongeza ukusanyaji wa mapato hayatakuwa na tija kwa Taifa kama Msajili wa Hazina hatoboresha njia bora ya kusimamia ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo hivyo.

## 4.3 Fungu 011 - Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji

(i) Kutokuwepo kwa usimamizi thabiti wa Kanda Maalumu za Kiuchumi kunapelekea uanzishwaji wa kanda hizo kutokuwa na tija iliyokusudiwa kwa Taifa; na

(ii) Changamoto ya elimu ya kutosha ya uwekezaji na fursa za uwekezaji kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi, inapelekea wadau hao kuwekeza katika maeneo na Miradi ambayo si ya kimkakati kwa Taifa.

## 4.4 Ushauri Mahususi Fungu kwa Fungu

### 4.4.1 Fungu 66 – Tume ya Mipango

(i) Serikali ihakikishe inaandaa nyenzo bora za Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2050 ili kuweza kulata Tija kwa wananchi;

(ii) Serikali ihakikishe ushiriki wa Sekta binafsi katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo nchini; na

(iii) Serikali ifanye tathmini na kuhusu miradi ya Kimkakati inayotekelezwa na inayotarajiwa kutekelezwa na Serikali ili kuhakikisha kwamba miradi hiyo inaleta Tija kwa wananchi na Taifa.

### 4.4.2 Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina

i. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe kwamba inaendelea na Uwekezaji katika masoko ya Hisa na Taasisi Binafsi zenye tija na manufaa kwa Taifa;

ii. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe inafanya tathmini ya mali zilizorejeshwa serikalini, kuziendeleza ili ziweze kuongeza mapato kwa Serikali.

iii. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina inasimamia uwekezaji wa umma ili kuongeza mchango wa Taasisi na Mashirika hayo katika kuchangia katika Mfuko Mkuubwa Serikali ili kukuza pato la serikali na Taifa kwa ujumla.

iv. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe kwamba inaweka makadirio ya makusanyo ya maduhuli yanayoakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vyake; na

v. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina inaboresha vyanzo vingine vya mapato ikiwemo madeni

yanayotokana na ubinafsishaji wa mali za Serikali ili kuboresha na kuongeza ukusanyaji wa mapato.

### 4.4.3 FUNGU NA 011- Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji

i. Serikali kusimamia uwekezaji wa kanda maalumu za kiuchumi ili kuleta tija kwa Taifa; na
ii. Serikali iendelee kutoa elimu ya Uwekezaji na fursa za Uwekezaji kwa wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi katika Kanda maalumu ya kiuchumi na miradi ya Kimkakati ya Taifa.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb.
9. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb.
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb.
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb.
12. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb.
13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb.
15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb.

17. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb.
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.
19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb.
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb.
21. Mhe. Aziza Seylum Ally, Mb.
22. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru, **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ambae pia ni Mwenyekiti wa Tume ya Mipango, Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo, (Mb) –Waziri Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Mhe. Stanslaus Haroun Nyongo,(Mb)- Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji Uwekezaji kwa ushirikiano ambao wameendelela kutoa kwa Kamati kwa wakati wote.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi hiyo pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Tausi Mbaga Kida, Ndg. Fred Matola Msemwa – Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango na Ndg. Nehemiah Kyando Mchechu - Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leornard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kiupekee nawashukuru Sekretarieti ya

Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb

**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

24 Aprili, 2025